

## **TAARIFA YA UJENZI WA SHULE YA MSINGI TARAJALI KAYENZE NDOGO (BUGOGWA B)**

### **UTANGULIZI.**

Ujenzi wa shule ya Msingi Kayenze ndogo ulianza **agosti 2016** kwa nguvu ya wananchi wakishirikiana na Mh. Diwani pamoja na Mbunge. Awamu ya kwanza ya ujenzi ilihusisha ujenzi wa msingi na boma. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi ilihusisha ujenzi wa veranda, ujenzi wa korido, uboreshwaji wa boma lililojengwa na wananchi, kushindilia moramu, kumwaga zege, kuweka madirisha, kujenga hanam, kupiga lipu ndani na nje, kuweka madirisha na milango, kupaka rangi ndani na nje, kuezeka, kuweka gypsum board na aluminium ofisi za walimu, kuweka mbao madarasani na kuweka vigae katika vyumba vinne vya madarasa na ofisi mbili za walimu. Aidha, shule imepokea jumla ya shilingi **66,600,000/= (pesa za EP4R)** ambapo hadi sasa fedha iliyotumika ni **44,903,000/=**.

Awamu ya tatu ya ujenzi inahusisha ujenzi wa matundu 10 ya vyoo. Katika hatua hii, nguvu za wananchi zina thamani ya Tsh. **1,880,000/=** na fedha ya serikali iliyopitishwa na inayoendelea kutumika ni shilingi **9,050,000/=**. Katika awamu hii tofali zitakazotumika ni za Mh. Mbunge. Awamu hii vilevile inahusisha ujenzi wa msingi wa vyumba viwili vya madarasa iliyogharimu shilingi **2,480,000/-** ambapo shilingi **2,100,000/=** ni nguvu za wananchi na ni shilingi **380,000/=** zimetolewa na serikali kuu kupitia **EP4R**.

### **MICHANGO WA WADAU MBALIMBALI**

Hadi sasa, **Mh. Mbunge** amechangia mifuko 40 ya saruji wakati wa ujenzi wa boma pamoja na tofali 5000 ambazo zimesaidia katika ujenzi wa mradi huu. Aidha, Halmashauri imeshiriki kikamilifu katika utekezaji wa mradi huu kwa kutoa wataalamu wa uhandisi majengo na idara ya elimu kwa muda wote wa utekezaji mradi hali ambayo imepelekea mradi kuendelea bila kusimama. Aidha, mh. Diwani amechangia nondo 10 na mifuko 10 ya saruji yenye thamani ya **Tsh. 370,000/=**

Katika fedha za **EP4R** zilizopokelewa, shilingi **58,953,000/=** zimeshatumika. Vifaa vyote vya ujenzi vikiwemo vya choo vimeshanunuliwa na zinasubiliwa tofali ili ujenzi uweze kukamilika. Aidha, katika fedha hizo, shilingi **7,647,000/=** ambazo hazijatumika zimetengwa kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa boma pamoja na kupaua vyumba viwili vya madarasa vinavyoendelea kujengwa. Hata hivyo zitahitajika fedha zaidi kwa ajili ya umaliziaji (finishing).

### **HITIMISHO**

Hadi kufikia hatua hii, mradi huu una thamani ya **Tsh.68,943000/ =** ambapo **Tsh. 3,980,000/=** ni thamani ya nguvu za wananchi, **Tsh. 58,953,000/=** ni fedha toka Kerikali Kuu, **Tsh. 5,640,000/=** ni mchango toka ofisi ya Mh. Mbunge (**tofali 5000 na mifuko 40 ya saruji**) na vifaa vyenye thamani ya **Tsh. 370,000/=** vimetolewa na mh diwani. Utakapokamilika, mradi huu unatarajiwa kufikia takribani **Tsh. 130,000,000**.